FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS KISWAHILI 10 QUESTION PAPERS



FORM 1 HOLIDAYS SMART PASS KISWAHILI TEN QUESTION PAPERS

Prefer Calling Amobi Group of Examiners

@ 0743 333 000 OR 0706 851 439

For Marking Schemes

N/B In Response to the Huge Costs Associated in Coming Up with Such/Similar Resources Regularly, We inform us All, MARKING SCHEMES ARE NOT FREE OF CHARGE. However Similar QUESTIONS, Inform of soft Copies, are Absolutely FREE to Anybody/Everybody. Hence NOT FOR SALE

by Amobi Group of Examiners.


CALL AMOBI GROUP OF EXAMINERS @ 0743 333 000 OR 0706 851 439 TO ACQUIRE :













FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 01

UFAHAMU

Runinga na Ulimwengu wa Leo

Siku moja nilikuwa hotelini kisiwani Lamu, au amu (kama wanavyokiita wenyeji) na rafiki yangu tukila wali na pweza. Aliingia mzee mmoja aliyefahamika kisiwani kwa ugwiji wake wa masuala ya lugha ya Kiswahili. Nilijiwa na hamu ya kumwuliza mzee huyo aliyepotea na kubobea katika Kiswahili, jinsi neno 'runinga' lilivyozuka.

"Ahh, hilo" alishangaa kwa sauti kabla ya kuendelea, kijana kaa kitako nikweleze. Mswahili wa kwanza alipokiangalia kile chombo alishangaa. Kilikuwa kinaeleza na kuweka wazi mbele ya macho yake habari za ajabu. Hizi zilikotokea. Ni kitu kama uvumi hivi, huku kwetu tunasema 'rununu' basi ule si wa kusikia bali ni wa kuona; yaani kwa macho ambayo zamani yaliitwa maninga. Basi ikawa rununu ya maninga; mwishowe runinga' alieleza mzee huyo kwa ufasaha mkubwa.

Kila ninapokiwaziza chombo kinachojulikana kama runinga au televisheni, kisa kile hufyatuka akilini na sura ya mzee huyo kunijia. Tangu kuvumbuliwa kwake mwanzo mwanzo wa karne ya ishirini, runinga imekuwa mojawapo wa vyanzo vikuu vya maarifa, taarifa, elimu na burudani kwa watazamaji. Kutokana na chombo hiki tunapata picha za matendo yanayotendeka kwenye maeneo yaliyoko mbali na tuishiko. Kinatufichulia majanga yanayowafika wenzetu kutokana na mbaa ya vita au njaa; huonyesha harakati za wanasayansi za kujaribu kuvumbua mambo mapya kwenye anga zetu. Aidha runinga hutusawiria matukio au ya kufurahisha. Runinga ni nyenzo muhimu ya kutuelimisha na hata kutuburudisha kutokana na vipindi vyake mbalimbali.

Vipindi vya runinga huwa ni ishara za elektroniki ambazo hutumwa kama mawimbi ya redio na vyombo vinavyojulikana kama setilaiti au kwa matumizi ya kebo ambazo hupitishwa ardhini. Setilaiti ina uwezo wa kubadilisha ishara hizo na kuwa sauti na picha zinazoambatana na sauti hizo.

Je, ushawahi kuwazia ni mambo yepi yanatokea katika studio za runinga hususan wakati wa kusomwa kwa taarifa ya habari? Aghalabu wakati wa kusomwa kwa taarifa ya habari ni sehemu ndogo sana ya studio inayoonekana. Asilimia kubwa huwa mefichwa pamoja na mashine za kila aina ambazo huhusika na uwasilishaji wa habari hizo. Aidha wahudumu wengine wanaohusika na majukumu mbalimbali kama udhibiti wa mwangaza, uekezaji wa wanaosoma kuhusu muda uliopo, mdhibiti wa kamera zionyeshazo picha mbalimbali anayekuza picha kuhakikisha picha zimeonekana vyema. Wapo wengine wanaoshughulika na majukumu anuai ambao hawaonyeshwi.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Mbele ya msomaji wa taarifa hizo huwa kuna televisheni ndogo ambayo haionekani na ambayo humwonyesha picha zinazoonyeshwa. Aghalabu hatuwaoni wasomaji wengi wa taarifa za habari wakisoma habari zao kutoka maandishi wazi. Hali hii inatokana na kuwepo kwa kielekezi-runinga ambacho anakitumia, Msomaji huyu husoma taarifa zake kutokana na maandishi yanayoonekana kwenye mulishi au kiwambo cha kielezi hicho. Maneno hayo hukuzwa kwa njia mbili mbele ya lensi za kamera na kuweza kusomeka vizuri. Yupo opareta ambaye kazi yake kuu ni kuhakikisha kuwa amedhibiti kasi ya maneno yanayoonekana kwenye kielekezi-runinga hicho. Pia msomaji wake akitumia kifaa maalum. Hata hivyo, msomaji huwa na nakala nyingine ya habari iliyoandikwa anayoweza kuisoma iwapo pana hitilafu fulani ya kielekezi-runinga.
Wataalamu wa chumba kikuu cha kuyadhibiti matangazo hutumia vifaa maalumu vya sauti kuwakumbusha watangazaji kuhusu vipindi vya kupumzika kwa ajili ya matangazo ya biashara au mabadiliko yoyote katika mpangilio wa kipindi Fulani. Huwapo pia wataalamu wanaohakikisha kuwa picha zinazopatikana kwenye runinga ni sahihi na zinakubalika. Kutokana na majukumu mbalimbali ya wanaohusika, watazamaji wanapata picha nzuri na sauti zinazoafiki picha hizo. Hii ni siri mojawapo ya siri nyingi ambazo zimefubwatwa na uvumbuvi wa kisayansi.
Kama watazamaji wa runinga labda tunaishia kukubaliana na Yule mzee wa Lamu kuwa chombo hiki kina maajabu ya macho. Maajabu hayo yanatuelimisha, kutujuza, kutukumbusha na kutufanya tushirikiane na wenzetu walio mbali sana katika matukio yetu. Masafa yaliyoko kati yao yanafupishwa kwa kuwa wanatujia kwenye vyumba vyetu kama nasi tunavyofanya huko kwao.

MASWALI

1. Ni nini chanzo cha neno ‘runinga’? **(al 2)**

2. Taja faida nne za runinga **(al 4)**

3. Tunaweza kutazama picha za runinga kutoka kwenye vituo mbalimbali vya televisheni. Ni njia gani ipi inayotuwezesha kutazama vipindi vya runinga? **(al 2)**

4. Wakati wa kusomwa kwa taarifa za habari kuna wataalamu mbalimbali wanaohusika. Taja watatu **(al 3)**

5. Je, kwa nini mara nyingi msomaji wa habari haonekani kusoma habari bali huongea akiangalia watazamaji tu? **(al 2)**

6. Taja michezo miwili ya kimataifa iliyo maarufu zaidi inayotangazwa moja kwa moja kupitia runinga kote ulimwenguni. **(al 2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MATUMIZI YA LUGHA

1. Taja ala nne za kutamkia sauti, mbili tuli na mbili sogezi **(al 4)**

2. Ni ipi tofauti kuu kati ya konsonanti na irabu **(al 2)**

3. Taja sauti mbili mbili ambazo ni: **(al 3)**

a) Vipasuo **b)** Nazali **c)** Viyeyusho

4. a) Maktaba ni nini? **(al 1)**

b) Taja aina mbili za maktaba **(al 2)**

5. Andika sentensi hizi kwa wingi **(al 2)**

a) Kifaru huyu ni mkubwa

b) Kijiti kikubwa kilitumiwa kumuua nyoka.

6. Weka shadda katika neno barabara kwa jinsi mbili na uonyeshe tofauti kimaana. **(al 2)**

7. Eleza maana ya kiimbo. **(al 2)**

8. Andika maneno mawili mawili yenye silabi zenye miundo hii: **(al 2)**

a) KKI

b) KKKI

9. Taja sifa zozote nne za lugha **(al 4)**

10. Kanusha sentensi hizi

a) Amekuwa akisoma kwa miaka miwili **(al 1)**

b) Tuliimba na kuvuna mahindi **(al 1)**

c) Amekuja **(al 1)**

11. Kamilisha methali hizi

a) _____si ndo ndo ndo **(al 1)**

b) Mkono mtupu _____ **(al 1)**

c) _____mpende **(al 1)**

12. Taja aina mbili za viambishi **(al 2)**

13. Sahihisha sentensi hizi **(al 3)**

a) Kitabu hii yangu nilinunuliwa na mama.

b) Kijana mwenye alisoma vizuri alituzwa.

c) Mtoto ambaye aliyepotea ni wa Kamau.

14. Kamusi humsaidia mwanafunzi kwa njia gani tatu? **(al 3)**

ISIMU JAMII

15.a) Eleza maana ya Isimu Jamii **(al 2)**

b) Taja mambo manne ambayo sajili lugha hutegemea. **(al 4)**

FASIHI (**Alama 15)**

1. Taja na ufafanue aina mbili kuu za fasihi. **(al 4)**

2. Fafanua dhima/umuhimu wa fasihi **(al 7)**

3. Taja tanzu nne za fasihi andishi **(al 4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 02

(I) INSHA **(ALAMA 20)**

Insha yako isipungue maneno 350.

Andika insha inayoafiki methali "Fadhila za punda ni mateke".

II UFAHAMU

SOMA UFAHAMU UFATAO KISHA UJIBU MASWALI (Alama 15)

Beata alikuwa msichana mrembo lakini alikuwa haambiliki, hasemezeki . Fauka ya hayo, alikuwa na tama isiyo na kifani.

Alipokuwa katika shule ya msingi, walimu na wazazi walimfunza umuhimu wa kuwa na maadili. Isitoshe, alifunzwa masomo vyema lakini akili yake ilikuwa butu. Akawa haingizi chochote cha maana ila uchafu wa fikira. Nyumbani nako hakuzingatia maonyo. Alikuwa hatulii.

Wakati fulani wa krismasi, Beata alipomaliza tu shule ya msingi, alikutana na mwanamume mmoja mliliwa na wasichana wengi;mtajika kwa mali na jina lake ni Mshikaji . Beata akadanganywa akadanganyika. Akatorokea kwa huyu Mshikaji ambaye alikuwa ameshawataliki wake wawili tayari. Akawa mke mlezi. Ikabidi awalee watoto waliobaki na baba yao baada yamanazao kutanzuka. Beata mwanzoni aliona raha, ingwa alikereka kuitwa mama kabla hata ya kumkopoa mwana wake mwenyewe. Aliwabeza waliokuwepo awali na akajiona kuwa yeye ndiye mchukuzi bora. Akadharau kuwa pakacha likivuja, nafuu huwa ni kwa yule mchukuzi. Aliwaona wenzake kama maua yaliyonyauka na lake ndilo kwanza linaonana na jua.

Muda si muda, akajikuta ana wana watatu kwa kipindi kifupi. Mumewe naye hakutulia na mambo ya nje. Akaimarisha nyendo zake za kiguu na njia, akipochoka, akiingia garini na kuikata mitaa. Beata aende wapi? Alifungika nyumbani ndi ndi Akamlea mwana huyu na Yule; wake na wale wa kambo. Vijisenenesenene vikazidi. Lakini akajaribu kuvumilia akidhani atazila mbivu, wapi! Alipoligema ilibidi alinywe. Siku zikaja na kupita. Beata akajuta kwa kutosikiliza wakuu na kumkimbilia mtu ambaye hata hakuwa anmuelewa vizuri. Pesa na raha alizokuwa amezikimbilia akawa anazisikia kama hadithi ndotoni. Kwao nako kukawa hakurudiki. Beata akawa majamzito tena kama kawaida akawa anaenda kliniki za wajawazito. Alipopimwa ikabainika kuwa ana ukiwi. Mtoto alipozaliwa akafariki. Yule mumewe akaanza kumnyanyasa.

Baadaya miaka mitatu, bwana Mshikaji, aliyekuwa akijitapa kwa unene na mali, akaanza kupotelewa na kiriba chake cha tumbo. Homa za hapa na pale zikaanza kumyemelea. Vipelevipele vikamsambaa mwilini. Hata akamsingizia Beata kuwa ni yeye aliyeuleta huo

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

ukimwi Ilikuwa ni wazi kuwa msambazaji alikuwa ni yeye bwana. Waliokuwa pembe za chaki waliujua ukweli ulipokuwa . Baadhi ya vidosho wake walishaanza kupukutika kama majani yafanyavyo wakati wa mapukutiko. Isitoshe, wengine walikuwa hoi vitandani wakiwa hawajui waingiao wala watokao. Ugonjwa wa kamata ulishawakamata. Mwisho akawa ni wa kulazwa na kutoka hospitali hizi na zile. Pesa zikawaishia, wakawa waya. Beata akawa hana budi kuviuguza vidonda ndugu vyake na vya mumewe. Hatimaye, mumewe akabwagwa chini na ukimwi na akafafo!

Si ndugu si marafiki, hawakumuelewa Beata. Waliamuona kama pweza aliyejipalia makaa makubwa ya moto makali. Ada za shule zikawa ni shida. Huruma ikwaingia watu. Watu wakasema. "Lisilobudi hutendwa." Wakaubeba mzigo kwa hiari yao. Wakawafanyia watoto harambee ya ada na peza za matibabu. Mwishowe Beata naye aliaga dunia akiwa bado mbichi kwa umri. Hata miaka ishirini alikuwa bado hajafikisha. Watoto ikabidi walelewe na wahisani. Hapo walimwengu wakaja kutambua ukweli kwamba, uzuri si hoja hoja ni tabia. Isitoshe mtu akikimbiliwa na kila mtu, ukimwi hatauepuka. Mtu akiupata, hufa. Anadidimiza watu wengi pamoja na familia yake. Jamii ilifunzwa pia kuwa unene si hoja. Hata watu vibonge huweza kuleta ukimwi. Basi, jamii hiyo ikaazimia kuwa wao hawatakuwa watumwa wa tabia iletayo ukimwi. Walitambua kuwa ukimwi unarudisha nyuma maendeleo na kuipakaza jamii mizigo isiyo tarajiwa. Nasi tutahadhari kabla ya hatari

1. Andika kichwa kifaacho kisa hiki **(ala.1)**

2. Ni jambo gani lililomkera Beata baada ya kuolewa na Mshikaji? **(ala.1)**

3. Toa sababu moja iliyomfanya Beata kuwadharau wenzake waliomtangulia kwa mshikaji? **(ala.1)**

4. Ni kwa nini Beata alianza kujuta? **(ala2)**

5. Toa sababu moja kuonysha kuwa Mshikaji ndiye aliyeusambza ukimwi **(ala.1)**

6. Kulingana na kifungu hiki taja hasara zinazoletwa na ukimwi. **(ala.3)**

7. Kwa nini walimu na wazazi hawangelaumiwa kwa yale yaliyompata Beata? **(ala,1)**

8. Andika maana ya: **(ala.5)**

i) butu

ii) Kope zikawa si zake

iii) Akiwa bado mbichi

iv) Kuzanzuka

v) Vijisenensenene.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MATUMIZI YA LUGHA

a) Taja aina mbili kuu za sauti.katika kiswahili **(ala.2)**

b) Taja:

i) Irabu za mbele. **(ala.2)**

ii) Irabu ya kati **(ala.1)**

iii) Irabu za nyuma **(ala,1)**

c) Kiungo ambacho hutetemaka na kutoa sauti huitwaje. **(ala.1)**

d) Viungo ambavyo hutumika katika utamkaji wa sauti huitwa je? **(ala1)**

e) Taja aina mbili za konsonanti. **(ala.2)**

f) Andika konsonanti tatu mabazo ni vipasuo. **(ala.3)**

g) Toa mifano miwili ya sauti za nazali/ving'ong'o. **(ala.2)**

h) Suati mwambatano nini? **(ala.1)**

i) Taja vipashio vine vya lugha. **(ala.4)**

j) Tenganisha neneo lifuatalo katika viambiu vyake mbalimbali. **(ala.3)**

k) Eleza maana ya:

i) Kiimbo **(ala1)**

ii) Shada **(ala.1)**

l) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi. **(ala4)**

i) Ukuta mbao ulianguka ni huu

ii) Mwanagenzi Yule amepita mtihani vizuri

m) Sentensi zifuatazo ziko katika nyakati / hali gani? **(ala.2)**

a) Otieno hula samaki kila siku

b) Yeye anaandika t kitabu

n) Tambulisha manene mbalimbali katika sentensi zifuatazo. **(ala.4)**

i) Mwanafunzi mvumilivu alisoma vizuri.

ii) Yule ameongea manene mengi

o) Taja

p) Kanusha sentensi ifuatayo. **(ala2)**

i) Nyumba hiyo ifafunfuliwa

j) Eleza matumizi ya 'Koloni'

Kisha utungie sentensi. **(ala.1)**

FASHI SIMULIZI (ala. 15)

1. Fasihi simulizi ni nini? **(ala.2)**

2. Taja na ueleze majukumu matano ya fasihi simulizi **(ala 8)**

3. Eleza tofauti tano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi **(ala10]**

4. Taja tanza nne kuu za fasihi simulizi . **(ala.4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 03

UFAHAMU ALAMA 15

Elimu

Ni dhahiri kabisa kuwa elimu ndiyo msingi wa maendeleo.Elimu ya ujuzi na maarifa humfaidi mtu kwa kila njia-kiuchumi, kisayansi, katika utafiti wa aina tofautitofauti na kwa kuinafidhi jamii kwa jumla.Bila elimu, maendeleo hayawezi kupatikana kamwe; kuyataraji ni kama kutumaini kupata kitu kwenye ombwe tupu.

Binadamu si kibonge au kidude kinachoweza kukaa bila chakula, mawasiliano na uhusiano kati yake na mazingira.Bila elimu, matatizo chungu nzima yatamkumba mwanadamu.Mifano ya matatizo haya ni kama vile ukosefu wa vyakula, hali duni ya mawasiliano, mmomonyoko wa udongo na hali nyingine za kuhuzunisha na kuaibisha.Maliasili yaweza kutumika tu iwapo pana ujuzi.

Mito, misitu na madini ni vitu ambavyo vinaweza kurahisisha mno maisha ya wananchi vikitumiwa kwa ujuzi.Kwa mujibu wa ukweli huu, kujua kusoma na kuandika, ambacho ndicho kiini cha elimu, ni jambo la lazima katika Maisha.

Elimu hurahisisha mawasiliano.Uwezo wa kupashana habari hutegemea ujuzi.Mawasiliano ni ya njia nyingi tofauti kama vile simu, barua, telegramu na njia nyingine.Nchi isiyo na mawasiliano bora ni kama jangwa lisilopitika.Kwa vile kila habari hugeuza hali Fulani ya Maisha, bila ujuzi wa kusoma na kuandika, mawasiliano hayawezekani.

Maandishi mengi huwa na uzito wa maana na mtu yeyote asiyejua kusoma na kuelewa hawezi kunufaika kupitia kwa maandishi ilhali ajuaye atasoma, aelewe na kutimiza wajibu wake wa ujenzi wa taifa.Wahenga walisema, fumbato mfumbie mjinga, mwerevu huling'amua, kwani mwenye macho haambiwi tazama.Ni wazi kwamba mwenye ujuzi wa kusoma na kuandika ndiye atakayeelewa mawazo ya wenzake yaliyoandikwa na kuyatumia katika harakati za ujenzi wa taifa.

Shuleni, wanafunzi hufunzwa kusoma na kuandika kusudi waweze kuchambua maandishi tofauti ili wawe na uwezo wa kujitegemea wenyewe kimaarifa.Kwa kuchambua maandishi tofauti, wanafunzi huelewa yale yafaayo na yasiyofaa katika jamii kwa kutumia mifano mizuri au mibaya ya wahusika katika kazi za kisanaa.Kwa njia hii, wanafunzi hupima kila hali kwa makini-yaani huwaza na kuwazua kabla ya kukata shauri kutenda lililo bora na la kuleta maendeleo.

Katika ulimwengu wa biashara, kujua kusoma na kuandika ni jambo muhimu kwa vile mfanyi biashara ni lazima achemshe bongo ili kazi yake isidhoofike na mwishowe aangamie kifedha.Ni

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

lazima biashara itunzwe isije ikadidimia na ufukara ukaingia.Ufanisi katika biashara zifanywazo na watu binafsi huchangia ufanisi katika nchi kwa jumla, kwa maana haba na haba hujaza kibaba. Kupitia kwa utafiti katika nyanja tofauti, wanasayansi huwahudumia wananchi kwa njia nyingi madhubuti. Bila ujuzi wa kusoma na kuandika, watafiti, marubani, manahodha, madaktari na wahandisi na wenye taaluma nyingine hawawezi kupatikana.Kila mjuzi huwa na jukumu lake katika kuchangia maendeleo nchini; ni lazima mhandisi arekebishe mitambo, daktari atibu watu, nahodha aongoze chombo na mwalimu afundishe.Wote wanahitaji elimu.
Kwa mujibu wa hali hizi zote, ni Dhahiri kuwa ujuzi wa kusoma na kuandika ni jambo la lazima iwapo vikwazo katika ujenzi wa taifa vitaondolewa ili tupige hatua kubwa kimaendeleo.

Maswali

a) Je, elimu ina faida gani kwa mtu? **Alm 2**

b) Taja aina nne za shida zinazoweza kumkumba mtu kutokana na ukosefu wa elimu. **Alm 4**

c) Ni nini hasa kiini cha elimu? **Alm 2**

d) Eleza maana kamili ya mawasiliano na utaje mifano minne. **Alm 3**

e) Mwandishi anamaanisha nini anapotumia methali ‘fumbsto mfumbie mjinga, mwerevu

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu. **Alm 2**

Madini

Ombwe

MATUMIZI YA LUGHA ALAMA 35

a) Sauti hizi hutamkiwa wapi? **Alm 2**

(i) /w/ (ii)/d/

b) Tofautisha kati ya irabu na konsonanti. **Alm 4**

c) Taja vikundi saba vya konsonanti kwa kutolea mfano ukizingatia hali ya mtetemeko katika nyuzi za sauti. **Alm 7**

d) Kwa kupigia mstari, onyesha viambishi awali na tamati katika neno lifuatalo. **Alm 2**

Anakochezea

e) Taja vipashio vya lugha. **Alm 2**

f) Eleza maana ya: **Alm 4**

i) Shadda

ii) Kiimbo

g) Unda neno lenye muundo ufuatao. **Alm 2**

KKIKKI

h) Weka shadda mahali pafaapo. **Alm 1**

(i) Marudio

(ii) Karatasi

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

i)Eleza maaana ya maneno yafuatayo: **alm 3**

Kiambishi

Kihisishi

Kiwakilishi

j) Sahihisha. **Alm 2**

nelson mandela, aliyekuwa rais wa afrika kusini, alifanya mashauri na mobutu sesseseko wa zaire.

k) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika wakati ujao. **Alm 2**

Mpwa wangu anafua nguo zake.

l) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. **Alm 2**

Mama anapika ilhali dada anaanika nguo.

m) Andika katika wingi **alm 2**

Baba anachimba kisima.

ISIMUJAMII ALAMA 10

Eleza majukumu yoyote matano ya lugha **alm 10**

FASIHI SIMULIZI ALAMA 20

1. Eleza dhima ya fasihi katika jamii. **(alm 10)**

2. Onyesha tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi **alm 10**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 04

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma nakala kisha ujibu maswali;

Huku tukiadhimisha siku yakina mama duniani, kuna haja ya kutafakari kuhusus nafasi ya wanawake katika jamii.

Kwanza kabisa tunAfaa kufahamu mama ni nani. Mama ni mtu yeyote wa kike ambaye hulea na kuonyesha familia na jamii mahitaji haya awe dada, nyanya shangazi, **Mfadhili** , Jirani miongoni mwa wengine ni mama kwa mujibu wa mkutadha huu.

Ni dhahiri kuwa mama wamekuwa wakitekeleza majukumu muhimu maishani mwa familia na jamii lakini kama punda, wengi wetu huishia kuwalipa kwa mateke.
Sio viongozi wa serikali, sio kina baba wala watoto: miongoni mwao kuna wale ambao wamejitolea kuto watambua na kuto waheshimu binadamu hawa wenye nguvu,uwezo na mapenzi. Kina mama na wanawake kwa jumla wamekuwa walengwa wakuu wa ghasia katika familia.
Katika familia, kwa mifano. Kina mama wengi mpaka leo wanapigwa na kuteswa na wanaume zao bila sababu. Wengi wao wameachiwa jukumu la kuwalea watoto hata baada ya kukubali mzingo huo mzito, wana chapwa kila siku.

Visa vya kina mama wanaorauka kila siku kwenda kutafutia wanao chakula na wanaporudi wanapigwa na waume pia hukaa ndee kuwasubiri wake wao watafute na kisha huwanyang'anya kibaba chao kuongezea kwa machozi.

Baadhi ya wanawake mpaka sasa wamesalia watumwa na waume ambao hutoa amri na hawatarajii maswali wala manung'uniko.

Haki za ndoa za kina mama zinaendelela kuvunjwa na mabwana zao ambao wame jigeuza **madubwana** pili, watoto, hasa wa kiume ambao hingiwa na kasumba za dhuluma kutoka kwa baba na jamii pia wamekuwa waki wakosea kina mama heshima bila kujali sio na hata kushuhudia kina mama wakipigwa na watoto wao wa kiume baada ya mzozano.

Watoto w akiume wamejaa utundu, kwa mfano, ni mzigo mkubwa kwa kina mama mbali na kuwa tishio kwa furaha na amani yao katika familia na jamii wengi wa watoto hao hukataa shule na

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

kujiunga na magenge ya wahuni ambayo hutumia dawa za kulevya na kila baada jya kulewa wao huishia kuwa chokoza mama zao.

Baadhi yao hutaka mambo yasiowezekana na kukosa kufanya wanachotaka huwa na matuzi nakichapo cha mbwa kwa mama.

Viongozi wa serikali na kisiasa pia wamekuwa wakijikosea heshima kwa kuendelezamateso ya akina mama. Baadhi yao hudai wanawake hawana haki ya kuongea mbele yao. Huku wengine waki washambulia wakati wa kampeni.

Maswali

(a) Pendekeza kichwa mwafaka cha taarifa hii **(ala.1)**

(b) kwa mujibu wa kifungu , ni nani anastahili kuitwa mama **(ala. 3)**

(c) Ni matatizo gani yanayowakabili mama. **(ala.3)**

d) Taja makundi mbali mbali yanayonyanyasa akina mama. **(ala.3)**

e) Eleza kwa nini mwandishi anafananisha kina mama na punda. **(ala. 2)**

f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(ala.2)**

(i) Mfadhili

(ii) Madubwana

MATUMIZI YA LUGHA.

a) ***Onyesha tofauti ya vitate hivi kwa kuvitungia sentensi.*** **(ala.2)**

(i) Shaka

(ii) Chaka

b) J***aza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi ifuatayo kwa viambishi vifaavyo.*** **(ala.2)**

Mgeni_____refu_____Li____kuja amendaliwa chakula_____tamu.

c) ***Katika sentensi ifuatayo tambulisha.*** **(ala.4)**

(i) Kivumishi _____ (ii) Kitenzi_____

(iii) Kiunganishi_____ (iv) Nomino_____

Wazee walijitahidi lakini walishindwa na vijana machachari.

d. ***Sahihisha sentensi ifuatayo il kuunda sentensi tatu sahihi.*** **(ala. 3)**

Mahali kwenyewe panavutia

e ***Fafanunua maana ya misemo katika sentensi zifuatazo*** **(ala.2)**

(i) Ali cheza kamari lakini jitihada zake za kushinda **ziliambulia Patupu.**

(ii) Kilimo bado ni Uti wa mgongo wa uchumi wetu.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

f ***Andika kwa maneno*** **(ala.2)**

(i) 11,001

(ii) 10,001

g ***Tunga sentensi kuonyesha maana tatu za neno <u>chunga</u>*** **(ala.3)**

h. ***Andika upya sentensi zifuatazo kwa ukubwa:***

(i) Pako na ngamia wanafaidi watu sana.

(ii) Mtoto alitishwa na mtu mrefu.

I ***Kamilisha sentensi zifauatazo kwa kutumia tashbihi mwafaka*** **(ala. 2)**

(i) Huyu cheruiyot hachezi na wenzake nje; anachungwa kama

(ii) Mtu huyu ni mchafu kama

j. ***Toa mfano wa nomino mbili mbili zipataikanazo katika ngeli zifuatazo.*** **(ala.2)**

(i) I_____ I _____

(ii) U_____ Zi _____

k ***Ainisha maeno yafuatayo ilikubanisha viambishi na mzizi.*** **(ala.4)**

(i) Alikupiga.

(ii) Walimchezea.

l ***Eleza sifa moja moja kuu ya vitamkwa vifuatavyo kisha utoe mfano:*** (**ala. 2)**

(i) Kimadende

(ii) Kipasuo.

m. ***Toa methali inayoafikiana na maelezo yafautayo;*** **(ala.2)**

Mtu anapokuwa, akipahama mahali hapaswi kupaharibu au kupatu kanisha kwa kuwa huenda atahit aji kurudi hapo.

n. ***Unganisha sentensi hizi kwa kutumia kirejeshi 'amba'*** **(ala.1)**

(i) Mwanafunzi amepita mtihani

(ii) Mwanafunzi ni mtiifu.

o. ***Kamilisha tanakali za sauti zifuatazo.*** **(ala.2)**

(i) Nyooka

(ii) Nyeusi

p. ***Andika kinyume cha vitenzi viliyopigwa mstari*** **(ala.2)**

(i) <u>Alikashifiwa</u> kwa kazi aliyofanya

(ii) Kuimba <u>kulifurahisha</u> hadhira.

q. ***Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo.*** **(ala.1)**

Bibi yake amefika.

r. ***Geuza sentensi zifuatazo kwenda kauli ya kitenzi ilizooyeshwa kweny e mabano*** **(ala.2)**

(i) Mhunzi anamhesabia mfinyanzi pesa (Kutendeana)

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FASIHI SIMULIZI.

(a) Eleza aina mbili za nyimbo **(ala. 4)**

(b) Eleza sifa tatu zinazo tofautyisha fasihi simulizi na fasihi andishi. **(ala6)**

c) Eleza dhana zifuatazo za fasihi simulizi: **(ala.6)**

(i) Visasili

(ii) Hurafa:

(iii) Hekaya.

d) Taja umuhimu nne wa fasihi.

e) Taja vipawa alivyohitajika kuwa navyo mtambaji wa hadithi. **(ala.3)**

f.) Vitendawili ni nini? Toa mfano wa kitendawili **(ala. 2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 05

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Nairobi, mji mkuu wa Kenya ,ni jiji Ia maajabu na mastaajabu chungu nzima.Nadhari ya mtu anayewahi kuingia jiji hili kwa mara ya kwanza huvutiwa na huo mshehenеko wa majumba ya fahari, marefu ajabu ,kiasi chaminazi mitano-sita ,iliyounganishwa kuelekea juu. mbinguni.

Jumba linalowavutia watu wengi ni lile Ia makongamano ya kimataifa Iiitwalo kwa Kiingereza Kenyatta International Conference Centre Jumba hili,hadi miaka michache iliyopita, ndilo lililokuwa refu zaidi mjini Jumba lenyewe- lina ghorofa ishirini na tisa hivi ,usipohesabu hilo pambo kama kofia kileleni mwake,linalojulikana kama mwavuli. Hata hivyo ,miaka michache iliyopita jengo hili lilipitwa urefu na Mnara wa Nyakati (Times Tower).Mnara huo hasa ni jumba linaloafiki lakabu yake ya kikwaruza mawingu.Jumba hili lina ghorofa zisizopungua thelathini na mbili.

Mbali na majumba haya mawili ,kuna majumba mengine zaidi ya ishirini katikati ya jiji ambayo ,japo mengine ni mafupi kiasi ,yana maumbo ya kustaajabisha kweli kweli.Hebu zingatia mwenyewe jumba Iiitwalo “mdomo wa kengele” au “bell —bottom” ambalo ni vioo vitupu ,toka chini hadi juu.Fauka ya ,umbo lake ni Ia kipekee ulimwenguni kote. Jumba hili lina kama miguu, kisha kiuno mithili ya kinu hivi japo si mviringo.Linapaa juu ,mbali sana ,likichukua umbo pana kuliko lilivyo chini;umbo Ia fua pana kama kengele.

Halafu rudia barabara .hizi hazina hesabu katikati ya jiji na ni pana, tena safi sana.Magari yanayotumia barabara hizi ni kochokocho,ya kila ama yanashindania nafasi,

Ajabu kubwa ya Nairobi hata hivyo ni idadi ya watu.Hakuna hasa anayejua idadi kamili ya watu wa Nairobi ,lakini sio kupiga chuku ninaposema kwamba ,hasa nyakati za kuelekea kazini asubuhi ,kwenda kula chakula cha mchana ,kuelekea nyumbani baada ya kazi na kuvuka barabara wakati wa msongamano, watu hukanyangana .Mtu anayesema kwamba watu wa Nairobi ni wengi kama chungu ,au kama mchanga wa ufuo wa bahari, hatii chumvi.

Watu wa Nairobi ,kwa tabia na mavazi, si kama watu wa kwingineko nchini Kenya .Watu hawa huvalia nadhifu sana.Wanawake ni warembo ajabu na hutengeneza nywele zao mithiIi ya

hurulaini peponi.Wengi huvaa suruali ndefu. Kucha zao na midomo yao hupaka rangi maridadi sana.Huzungumza Kiswahili na Kiingereza takriban wakati wote.Wanawake wengi ajabu huendesha magari yao wenyewe ,jambo ambalo litakushangaza mara tu uingiapo jijini ,hasa kama ulilelewa ukidhani maskani mwafaka ya wanawake ni jikoni peke yake;yaani kuzingatia ile falsafa kuwa "kuoa ni kupata jiko".Wanaume nao huvaa suti safi ,maridadi na shingoni wamefunga tai stahiki yao.Wanaume hao huendesha magari na kuyaegesha karibu na afisi zao.Huingia afisini mwao kwa maringo na madaha,huku funguo za magari yao zikining'inia vidoleni. Hawa nao husema na Kiingereza kupitia puani, utadhani ni waingereza hasa.

Kwa upande mwingine ,watoto ni nadhifu kweli kweli hasa watoto wa shule.Hawa huvalia sare zilizofuliwa na kunyoshwa vizuri kwa pasi. Wake kwa waume ,shingoni huvalia tai Watoto wa shule za Nairobi huongea Kiswahili, Kiingereza na sheng,ambayo ni "lahja" yao waliyoibuni."Lahja" hii ni mchanganyiko wa Kiswahili,Kingereza na msamiati mchache wa lugha nyingine za Wakenya zisemwazo jijini Nairobi na vitongoji vyake.

Kwa jumla ,watu wote wa Nairobi hutembea kasi sana.Hawana hata wakati wa kutembea polepole na kuangazaangaza huku na huko.lwapo wewe ni mgeni jijini,ukizubaa utapigwa kumbo na waendelee na hamsini zao kama vile hapakutokea jambo.Hili linapojiri, usidhani limefanywa maksudi.La, hasha.Ni vile tu kwamba Wanairobi hawana muda wa kupoteza.

Maswali

(a) Kwa nini majumba ya jiji la Nairobi yana majina au lakabu za Kiingereza? **(ala 2)**

(b) (i) Baadhi ya maajabu ya Nairobi ni barabara safi, msongamano wa magari na majumba marefu. Ongezea maajabu mengine matatu. **(ala 3)**

(ii) Watu wa Nairobi wanajipenda kweli kweli, Fafanua **(ala 3)**

(c) (i) Je, Unadhani watu wa Nairobi kweli hukanyagana? Eleza ni kwa nini msimulizi ametoa maelezo hayo **(ala 1)**

(ii) Unafikiri ni kwa nini hasa wanawake wa Nairobi wanaonekana nadhifu? **(ala 2)**

(d) Kwa nini neno "lahja" limewekwa alama za mtajo? **(ala 1)**

(e) Eleza maana ya maneno na tamathali za usemi zifuatazo. **(ala 3)**

(i) Nadhari

(ii) Linaloafiki

(iii) Waendelee na hamsini zao

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

2. UFUPISHO

Kiswahili nchini Kenya kilisambazwa kwa njia ya biashara kutoka upwa wa Kenya kwenda bara yake ,ingawa si kwa wingi sana kwa sababu wenyeji wa upwa wa Kenya —Mombasa, Siu na Pate-walikuwa katika vita vya kupigana na utawala wa Kisultani wa Seyyid Said, Sayyid Majid na Seyyid Barrgash.Hata hivyo kuna baadhi ya misafara iliyokwenda bara na kueneza Kiswahili.Kwa mfano, Waswahili wa kutoka Jomvu na Mvita walifanya biashara na Wakamba.Baadhi yao walioa Ukambani na mpaka wa leo kuna milango ya Waswahili ambao nyanya zao wanatoka Ukambani.Wafanyabiashara wengine Waswahili walifika mpaka Umaasaini.

Utawala wa kikoloni ulikitweza sana Kiswahili. Waingereza walitilia mkazo utumiaji wa lugha za kikabila kwa vile walisema kwamba mtu angeeleza hisia zake vizuri kwa kutumia lugha yake ya kwanza.Kiswahili kilitwezwa na kuchukuliwa kuwa ni lugha ya maboi.Wajerumani walikitweza sana nchini Kenya.Wamisheni pia walikipinga Kiswahili kwa sababu ya ufungamanao na Uislamu,

Hata hivyo, Kiswahili kilikuwa kinatumika katika mawasiliano, kwa hivyo wakakata shauri kwamba kitumike katika kufundashia shuleni.Lugha za makabila zilitumiwa katika madarasa ya chini-Kiswahili katika madarasa ya kati, na Kiingereza katika madarasa ya juu.Mtihani wa Kenya African Preliminary Examination (KAPE), ulikuwa ukifanywa katika lugha ya Kswahili nchini Kenya, uliondolewa,

Kiswahili kilitumika katika kuwaunganisha wakenya katika shughuli za ukombozi wa nchi na pia kama lugha ya umma.Mnamo mwaka wa 1964,Tume ya Ominde ilipendekeza kwamba Kiswahili kitumike kwa vile ndiyo lugha ya kumuunganisha Mwafrika, na pia ingetuwezesha kuwasiliana na nchi zingine za Afrika Mashariki na Kongo,

Mnamo mwaka wa 1969, chama cha Kenya National Africa Union (KANU) ,kilifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa, Raisi wa kwanza wa KANU alikuwa akitolea hotuba zake nyingi katika lugha ya Kiswahili, na alitoa kwa Kiingereza kwa ajili ya mabalozi tu.Fasihi ya Kiswahili ilianzishwa mwaka wa 1973, na kwa hivyo wanafunzi wakaanza kuifanya katika kidato cha nne na cha sita.

Ingawa Kiswahili kilitwezwa sana na Waingereza, bado kinatumika na watu wengi kama lugha ya mawasiliano.Mwaka wa 1968, Berndt Heine alifanya uchunguzi na aliona kwamba asilimia 85.25 ya Wakenya hutumia Kiswahili kama lugha yao ya pili na ndiyo lugha ya mawasiliano.Hivi

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

sasa lugha ya Kiswahili imepewa kipaumbele;ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi.Katika sekta ya elimu,Kiswahili ni somo Ia lazima katika shule za msimgi na za sekondari.Ni somo ambalo linanaendeelezwa hata katika vyuo vikuu vya Kenya.

Ni muhimu kutaja kuwa Kiswahili hakikuenea katika bara ya Kenya kama kilivyoenea Tanganyika. Kiswahili kilienea sana Tanzania kwa sababu ya wakoloni, yaani Wajerumani,waliosisitiza matumizi ya Kiswahili;lakini Waingereza walikitweza katika nchi ya Kenya
Licha ya hayo,nchi ya Tanzania ina lugha 120, na Kenya ina lugha kama 41.Nchi ikiwa na lugha nyingi na watu wachache wanaoitumia kila mojawapo ya lugha hizi,ni rahisi kukuza au kuinua lugha moja kuwa lugha ya taifa inayotumiwa na watu wengi.Hoja hii ilifanya Kiswahili kisienee sana Uganda na Kenya ,lakini kikaenea sana Tanzania.

Kiswahili hakikuenea sana nchi ya Kenya kwa sababu biashara haikufana sana katika pwani ya Kenya kama mji wa Unguja.Wanyamwezi na Wayao waliokuwa wakishughulika na biashara huko Tanzania walieneza Kiswahili katika bara, jambo ambalo Wakamba walioshughulika na biashara Kenya hawakushughulika nalo.Wakamba hawakuiga lugha ya watu wa pwani,Wamaasai waliogopwa sana na wafanyabiashara,na kwa hivyo biashara haikufana sana.

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa fupisha aya ya kwanza na ya pili (maneno 50-60) **(ala 7)**
Nakala chafu
Nakala safi

(b) Kwa kuzingatia aya za mwisho, eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi (maneno 60 – 70) **(ala 8)**
Nakala chafu
Nakala safi

MATUMIZI YA LUGHA

(a)(i) Eleza tofauti kati ya sauti /z/ na /d/ **(ala 1)**

(ii) Toa kigezo chochote kimoja cha kuainishia konsonanti. **(ala 1)**

(b) Sentensi ifuatayo ina maana mbili tofauti. Zieleze. **(ala 2)**
Huyu amekuja kutuliza.

(c) Ikanushe sentensi ifuatayo kwa udogo. **(ala 2)**
Nyumba yenyewe ilijengwa bondeni karibu na mto.

(d) Onyesha shadda katika maneno yafuatayo: **(ala 2)**
(i) Mbono (mti) **(ii)** Barabara (sawasawa)

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(e) Andika sentensi kuonyesha matumizi mawili ya:

(i) Kinyota **(ala 2)**

(ii) Ritifaa . **(ala 2)**

(f) Tunga sentensi mbili tofauti zinazobainisha maana tofauti kati ya **(ala 2)**

(i) Nduni **(ii)** Duni

(g) Taja aina zozote mbili za sentensi. **(ala 2)**

(h) Andika sentensi ifuatayo iwe katika hai ya -ki- ya masharti **(ala 2)**

Tulilala sana tukachelewa kwenda shuleni.

(1) Taja aina nne za nomino**.** **(al2)**

(2) Tambua aina za vihusishi vilivyo pigwa mistari katika sentensi zifuatazo. **(al2)**

(a) Hassan anacheza vizuri **<u>kuliko</u>** Kiprini.

(b) Simtambui **<u>kwa vile</u>** amebadilisha nguo.

(j) Taja ngeli za nomino zifuatazo **(ala 3)**

(1) Ujinga **(3)** Kucheza **(5)** Barua

(2) Ugonjwa **(4)** Sukari **(6)** Mti

(k) Tunga sentensi ukitumia nomino ifuatayo pamoja na kivumishi kisisitizi cha mbali kidogo, Mgomba **(ala 2)**

(l) Tunga sentensi mbili ukitumia neno <u>kisabuni</u> kama: **(ala 2)**

(i) Nomino

(ii) kielezi

(m) Andika visawe vya **(ala 2)**

(i) Hidaya

(ii) Ngeu

(n) Iandike sentensi ifuatayo upya ukitumia ‘0” rejeshi tamati **(ala 2)**

Chumvi iliyochafuka si ile unayoizungumzia.

(o) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo **(ala 2)**

Mwanasiasa shupavu aliyewachochea wananchi amekamatwa.

(p) Yakinisha sentensi ifuatayo katika umoja **(ala 2)**

Nyuzi zisingekatika zisingepotea.

(q) Taja matumizi ya kiambishi ku_ **(ala 1)**

(r) Taja aina mbili za mofimu **(ala 2)**

4. ISIMU JAMII

a. Taja sababu mbili zinazomfanya mzungumzaji kutumia zaidi ya lugha moja katika mazungumzo **(ala 2)**

b. Kwa kutoa mfano, eleza maana ya uwingi lugha. **(ala 2)**

c.Fafanua mambo sita yanaoweza kuifanya lugha yeyote ife, **(ala 6)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 06

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali yanayofuata

Madhara ya sigara

Chimbuko la kuonekana kwa madhara ya tumbaku ilikuwa mwaka 1598 A.D. Madhara yake yaligundulika wakati ambapo makala ya kwanza ya kiafya iliandikwa nchini Uingereza ikieleza madhara ya sigara. Baada ya hapo zilifuatia tafiti mbalimbali zilizoendelea kugundua na kuelezea madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa za tumbaku kwa binadamu. Matokeo ya tafiti hizo yaliwezesha baadhi ya nchi kama vile Denmark, Uholanzi na Sweden kutunga sheria zinazozuia matumizi ya sigara. Katika sura ya pili, baadhi ya serikali zilikwazwa kiuchumi kwa kukosa pato la kodi zitokanazo na sigara na bidhaa zingine za tumbaku.

Mashirika na kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji na uuzaji wa sigara hutenga fungu kubwa la fedha kwa ajili ya kutangaza bidhaa hiyo hatari kwa afya ya mwanadamu. Kila mwaka, Shirika la Afya Ulimwenguni hutenga siku maalumu ya kuelimisha jamii kuhusu athari za kiafya na madhara yatokanayo na matumizi ya tumbaku. **Maadhimisho** hayo hufanyika kila Mei 30 ya mwaka na kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa “Mkinge mwanamke kuwa mteja au kutumiwa kama mhamasishaji wa bidhaa zingine za tumbaku’.

Takwimu za shirika hilo zinabainisha kuwa asilimia 90 ya wavutaji sigara wameanzia umri wa miaka 18. Pia zimebainisha kuwa, kwa kila sekunde ipitayo, wastani wa mtu mmoja anafariki kutokana na madhara ya tumbaku. Inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2025, vifo vitaongezeka kwa asilimia 70. Utafiti umebainisha ifikapo mwaka 2030, watu milioni 10 watakuwa wamefariki kutokana na kuvuta sigara.

Uvutaji sigara unasababisha magonjwa mengi kama vile saratani ya mapafu, wendawazimu, **kupooza,** matatizo ya mfumo wa hewa, kutoboka utumbo, kunyonyoka nywele, kupungua kwa nguvu za kiume, maradhi ya ngozi na kadhalika. Madhara ya tumbaku hayajitokezi mara moja. Huchukua kipindi kirefu hata miaka 30, hali inayowafanya wengi kufumbia macho tahadhari iliyopo, wakiendelea kuteketezwa na uvutaji sigara. Anayevuta sigara huathirika mapafu kutokana na moshi na tindikali – aina ya kaboni iliyomo kwenye tumbaku inayomzuia kupumua

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

na mapafu yake huanza kutunga usaha. Hali hiyo huchangia mtu kupata athari nyinginezo kama vile kichomi, kifua kikuu na saratani. Chembechembe ya nikotini iliyomo katika tumbaku ni hatari kwa mvutaji kwani humpotezea mtu hamu ya kula na anapata maumivu makali ya tumbo.

Wakati wote, mvutaji sigara hutoa harufu mbaya mdomoni, hali ambayo haipendezi katika maisha ya mwanadamu, na pia, huwa anawadhuru wengine. Mtu huyo anapopumua huchafua mazingira kwa kupumua hewa chafu na mbaya zaidi ambayo huwadhuru watu walio karibu naye kama vile mwenza katika ndoa (mke au mume), watoto au marafiki.

Inaelezwa kuwa sigara huathiri akili ya mwanadamu kutokana na kuwepo kwa chembechembe za ulevi. Hali hiyo ipo zaidi mtu anapotumia sigara kwa mara ya kwanza kabisa. Utafiti wa kitaalamu umethibitisha watoto wanaolelewa katika mazingira ya wazazi wanaotumia sigara kuathirika mishipa inayosafirisha damu kwenda katika moyo. Hali hiyo husababisha kuharibika kwa mfumo wa usafirishaji damu mwilini kwa watoto hao na mwishowe wanakuwa wahanga wa maradhi tofautitofauti.

Katika sura ya pili ya kisaikolojia, watoto wanaokaa na wazazi wanaovuta sigara huishia kuifuata tabia hiyo na huo ndio huwa mwanzo wa kudhoofika kwa maadili. Kwa wajawazito, sigara ina madhara kama vile kuathiri ukuaji wa mimba na kondo la nyuma au *placenta* kwa Kiingereza na kushindwa kusafirisha chakula vizuri kutoka kwa mama kwenda kwa moto. Madhara mengine ni moto kuzaliwa na uzito pungufu, hivyo kuathiri ukuaji wake. Kwa hivyo, ni vyema kufahamu kuwa ingawa sigara ni bidhaa inayotumiwa kama uraibu wakati wa kuivuta, madhara yake ni janga kubwa linalopaswa kupigwa vita bila kuchoka.

Maswali

(a) Madhara ya sigara yalionekana mwaka gani ? **(alm1)**

(b) Ni nchi gani zilizokuwa za kwanza kubuni sheria mpya kuhusu uvutaji wa sigara ? **(alm1)**

(c) Uvutaji wa sigara una athari gani kwa anayevuta ? **(alm5)**

(d) Watoto wanaathiriwa vipi na sigara ? **(alm4)**

(e) Thibitisha kwamba uvutaji sigara hugharimu pesa nyingi. **(alm2)**

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatayo kama ulivyotumiwa katika kifungu. **(alm2)**

(i) Kupooza

(ii) Maadhimisho

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

LUGHA - SEHEMU B

(a) Kwa kuzingatia jinsi ya kutamka sauti za kswahili ni nini tofauti kati ya **(alm2)**

(i) Irabu

(ii) Konsonanti

(b) Eleza maana ya dhana hizi **(alm2)**

(i) Kiimbo

(ii) Shadda

(c) Taja vipashio vine vya lugha **(alm4)**

(d) Andika sentensi zifuatazo katika hali timilifu **(alm2)**

(i) Mabati yananunuliwa

(ii) Baba atakwenda dukani

(e) Kanusha sentensi zifuatazo **(alm3)**

(i) Nchi za Afrika mashariki zalemewa na madeni.

(ii) Mbu amemuuma mtoto.

(iii) Baba ameandika barua ndefu.

(f) Zigeuze sentensi zifuatazo ziwe katika wakati uliopita **(alm2)**

(i) Unapendelea kula nyama siku hizi.

(ii) Opiyo alipenda kujiingiza katikati kama mchuzi wa ugali.

(g) Andika kwa wingi **(alm2)**

(i) Maziwa ya mtoto yalimwagwa na paka yule.

(ii) Uvivu wa Juma unakera.

(h) Akifisha sentensi zifuatazo **(alm2)**

(i) nenda sokoni ukaninunulie sukari maziwa na mkate

(ii) Maadam umeshafika tuanze mkutano

(j) Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kuandika viambishi mwafaka kulingana na kitenzi (alm5)

Kitenzi	Nafsi	Wakati	Kirejeshi	Kitendwa	Mzizi	kiishio
Aliyelima						
Aliyempiga						
Anaoupanda						
Alipika						
Nitavileta						

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

(k) Taja vipera vya fasihi simulizi **(alm 2)**

(l) Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo **(alm 2)**

Mama amepika chai tamu sana

Nitakutembelea kesho jioni

(m) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendwa **(alm4)**

(i) Piga -

(ii) Jenga –

(iii) Fagia –

(iv) Chora -

(n) Taja na ueleze dhima ya lugha **(alm2)**

(o) Andika sentensi zifuatazo katika hali ya mazoea **(alm2)**

(i) Mchoraji yule anachora picha nzuri

(ii) Mpishi atapika chakula kitamu

(p) Bainisha maneno katika sentensi zifuatazo. **(alm4)**

Salaala ! Majangili wamewaua ndovu kumi leo asubuhi

Wale watafungwa

FASIHI (ALAMA 15)

(i) Taja majukumu matano ya fasihi ya kiswahili **(alm5)**

(ii) Taja tofauti ya fasihi simulizi na fasihi andishi **(alm10)**

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Nunua sabuni mpya ya GRESHA. *It is new !* Harufu yake ni *poa*, inadumu siku yote, inalainisha ngozi. Ng'arisha nguo zako na sabuni ya GRESHA. GRESHA sabuni *poa !* Bei yake ni nafuu; shilingi 20/= tu. Kila mtu ainunua.

Maswali

(a) Hii ni lugha gani ? **(alm2)**

(b) Eleza sifa za lugha hii. **(alm8)**

Insha (Aalama 20)

Andika insha itakayomalizikia kwa maneno haya ……. "Nilipopokea mezani chakula kitamu nilikumbuka maisha magumu niliyoyapitia, nikatambua kuwa si rahisi kupata chakula kama hicho bila juhudi maishani."

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 07

1. INSHA: (Alama 20)

Andika barua ya kuomba nafasi ya kujiunga na shule ya upili baada ya kupita mtihani wa darasa la nane.

2. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo halafu ujiu maswali

UMOJA NA UTANGAMANO WA KITAIFA

Taifa ni jamii ya watu wanaoishi pamoja na kuunganika kihistoria na kitamaduni chini ya serikali moja. Muunganiko huu hutokea kinasibu na watu kujikuta chini ya himaya moja. Umoja na utangamano katika taifa hutokana na mambo kadha wa kadha.

Kwanza kabisa ni ushirikiano baina ya wanajamii wenyewe. Umoja wao huletwa na lugha wanayotumia. Hapa nchini Kenya Kiswahili kimechangia pakubwa katika kuleta utangamano. Luhga ya Kiswahili inazungumzwa kote nchini. Wananchi kutoka sehemu tofauti za nchi wanaweza kuwasiliana bila shida yoyote.

Pili, utawala wa serikali ya kitaifa huleta utangamano wa jamii katika nchi. Huduma za serikali hutolewa kwa wote bila ya ubaguzi. Nchi inapokuwa chini ya kiongozi aliyechaguliwa na wananchi hufanikisha umoja.

Jambo lingine ambalo huleta utangamano wa kitaifa, ni kuweko kwa sera inayoongoza maazimio na malengo ya taifa. Viongozi na wananchi wote hujitahidi kuchangia katika kuyafikia maazimio na malengo ya taifa lao.

Utamaduni wa nchi nao ni muhimu katika kuleta umoja wa kitaifa. Mila, itikadi na kaida zenye manufaa na zinazokubalika na jamii hufanikisha kutambulisha taifa. Hivyo wananchi kupigania kwa jino na ukucha kuhifadhi utamaduni wao. Kwa mfano: sanaa za uigizaji na uimbaji nchini Kenya husaidia kutomelea umoja huu. Tamasha hizi ni chombo muhimu cha utangamano. Mfumo sawa wa elimu nchini ni njia nyingine ya kuimarisha umoja wa kitaifa.

Wafanyibiashara wanaposafiri kutoka sehemu moja ya nchi hadi nyingine hutangamana na wananchi wenzao wanapouza au kununua bidhaa na huduma. Utangamano huo hukuza umoja wao.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Maswali

a) Eleza maana ya taifa. **(al 2)**

b) Eleza umuhimu wa Kiswahili nchini Kenya. **(al2)**

c) Taja mambo manne ambayo huleta umoja wa kitaifa. **(al4)**

d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa kifungu hiki. **(al 2)**

i) Utangamano **ii)** Utamaduni

3. Matumizi ya lugha ***(al. 30)***

a) Taja sifa mbili mbili za sauti zifuatazo. (al. 4)

i) /u/ **ii)** /e/

b) Yaja sauti mbili mbili ambazo ni, (al. 6)

i) Vipasuo **ii)** Nazali **iii)** Vikwamizo

c) Pambanua aina za maneno katika sentensi ifuatayo**.** **(al. $2^1/_2$)**

Maharagwe yalivunwa na kutiwa ghalani.

d) Panga maneno haya vizuri ili yaunde sentensi sahihi**.** **(al. 2)**

Hodari Yule mwanamuziki nchi amezuru nyingi Afrika za.

e) Tunga sentensi moja moja kubainisha maana ya maneno yafuatayo; **(al.2)**

i) Paa **ii)** Shuka

f) Kanusha sentensi ifuatayo; **(al. 2)**

Mwalimu anasahihisha kitabu cha mwanafunzi.

g) Andika sentensi ifuatayo upya ukizigatia maagizo kwenye mambano. **(al. 2)**

Mazingira yamehifadhiwa. (hali ya mazoea)

h) Maneno yafuatayo hupatikana katika ngeli zipi? **(al. 2)**

1. Manukato **2.** Sukari

i) Tofautisha sentensi hizi. **(al. 4)**

1. Gari liliibwa **2.** Gari liliibiwa

j) Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia vitenzi vilivyo katakia mambano. **(al. 2)**

i) Sauti hii ili ……..na fuudi wa kihindi. (shone)

ii) Yuko wapi Yule mgonjwa aliye…….. hapa? (leta)

k) Eleza maana ya msamiati ufuatao wa ushairi. **(al. $2^1/_2$)**

i) Ubeti **ii)** Mizani **iii)** Mshororo **iv)** Ukwapi **v)** Dhamira

4.ISIMUJAMII (al 10)

a) Eleza maana ya;

i) Isimu **ii)** Jamii **iii)** Isimujamii **iv)** Sajili **v)** Lafudhi

5.FASIHI SIMULIZI. **(al 10)**

a) Eleza maana ya fasihi. **(al. 2)**

b) Toa sifa nne ili kutofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi. **(al. 8)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 08

SEHEMU YA A: INSHA ALAMA 20

Andika insha itakayoanza kwa:
Tuliamka asubuhi ya majogoo tayari kwa safari tuliyoingojea kwa siku nyingi…

SEHEMU YA B : UFAHAMU B ALAMA 20

Mavazi Rekebisheni

Vazi jema kivaliwa, huongeza heshima,
Staha mtu kapewa, pote endapo daima,
Mavazi duni si sawa, kina dada ninasema,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Longi kwa nyuma kushika, na mapajani kubana,
Chupi zilipowafika, dhahiri kuonekana,
Bure munaaibikia,na kujishusha maana,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Kifuani kujikaza, maziwa yaning'inie,
Kitu gani munawaza, hamna habari nyie,
Ni ashiki mwasambaza, sikizeni niwambie,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Msichana ni hatia, magotini kufichuka,
Hivyo basi kuvalia,rinda lisoyafunika,
Huenda zusha hisia, maovu yakawafika,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Kuwa wazi kinenani, hupendeza Baniani,
Kwao mila ya zamani, si kujitakia shani,
Weusi twatafutani, kuiga za Ulayani,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Sitakosa kuzitaja, skati mnazovaa,
Zaisha kwa mapaja,kikiri kuchuchumaa,
Iko wazi nyonga moja, mkato ulivyokaa,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Wazi nitawasomea, nguo hizi nguo gani ?
Dada zetu mwakosea, kuzivaa hadharani,
Ndizo hizo huchochea, usherati mitaani,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Nguo chini zishusheni, mwilini mzipanue,
Heri kuingia deni, za heshima mnunue,
Kuigiza za kigeni, ni utumwa mtambue
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

Beti tisa namaliza, kalamu naweka chini,
Iwapo wajiuliza, nakereketwa ni nini ?
Ni staha nahimiza, sio wake kuhaini,
Mavazi rekebisheni, usherati umezidi.

a) Shairi hili ni la aina gani? **(alm1)**
b) Shairi hili lina beti ngapi? **(alm1)**
c) Eleza vina vya ubeti wa kwanza . **(alm1)**
d) Shairi hili lina kibwagizo au kimalizio? Kwa nini ? **(alm1)**
e) Taja tatu nne za mavazi ambazo msanii ana kashifu. **(alm3)**
f) Kwa kuzingatia maudhui ya shairi hili , fafanua methali : **(alm2)**
Chema chajiuza, kibaya chajitembeza.
g) Eleza umbo la shairi. **(alm4)**
h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi**.** **(alm3)**

i) Staha
ii) ashiki
iii) twatafutani

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MATUMIZI YA LUGHA C: (alama 35)

a) Toa tatu mbili za irabu **i** **(al3)**

b) Taja sauti mbili ambazo ni vipasuo vya ufizi **(al2)**

c) Eleza maana ya silabi kwa kutolea mfano **(al2)**

d) Maneno yafuatayo yana silabi ngapi? **(Al2)**

i. Maktaba

ii. Mwanafunzi

e) Unda neno moja lenye sauti mwambatano **(al1)**

f) Andika sentensi zifuatazo bila ya kutumia kirejeshi amba---- **(al2)**

Fulana ambayo imefumwa ni nyekundu

g) Tunga sentensi mbili kudhihirisha tofauti kati ya: **(al4)**

i. Tata

ii. Dada

h) Taja vipashio vine vya lugha. **(al4)**

i) Andika sentensi hii katika ukubwa wingi **(al2)**

Mtu mrefu alianguka pu!

j) Bainisha maneno katika sentensi ifuatayo**.** **(al3)**

Mzazi ataenda mjini.

k) Ainisha viambishi katika sentensi. **(al2)**

Nilikimbia

l) Toa matumizi mawili ya mkwaju (/). **(al2)**

m) Weka maneno yafuatayo katika ngeli zao. **(al 3)**

i. Mbuyu

ii. Kifaru

iii. Chai

n) Sahihisha sentensi ifuatazo. **(al 1)**

Huko ndimo alimopatikana.

o) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika wakati ujao. **(al 1)**

Mimi ninapenda mtoto mtiifu

p) Andika wingi wa: **(al2)**

Mtoto ataenda shuleni.

q) Kanusha **(al1)**

Nitaruka kamba.

r) Panga maneno haya ili kupata sentensi sahihi

Mbegu mkulima nyingi amepanda**.** **(al 2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

SEHEMU D:ISIMUJAMII. [ALAMA 10]

a) Eleza maana ya sajili ya lugha. **[alm2]**

b) Taja mambo manne yanayosababisha kuibuka kwa sajili tofauti. **[alm4]**

c) Huko ukitoa mifano eleza sifa nne za sajili ya sokoni. **(alm4)**

SEHEMU YA E: FASIHI ALAMA 15

a) Fafanua aina mbili za fasihi **(alm2)**

b) Eleza sifa nne za mtambaji bora **(alm4)**

c) Eleza aina mbili za ngano **(alm2)**

d) Taja sifa tatu za fasihi simulizi **(alm4)**

e) Fafanua aina tatu ya wahusika katika fasihi simulizi. **(alm3)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 09

MAAGIZO

(a) Jibu maswali yote katika; Ufahamu, Ushairi, Matumizi ya lugha, fasihi simulizi na Isimujamii.
(b) Andika majibu yako katika nafasi uliyopewa

SEHEMU A: UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.
Jukwaani chini kulia kuna mlango wa kutokea. Linapofunguka pazia, Mama Tatu anaonekana akisuka ukili. Anaelekea mlango wa kutokea nje. Mlango wa kuingilia ndani upo upande wake wa kulia.
Mama: *(Anamtazama bila kupendezewa). Anasema huku anasuka ukili)* Hmm. Hiyo kanzu imezidi tena. Si unatembea uchi hivyo. Fupi, fupi, imekubana. Ndio uambiwe nini? Mzungu sana!
Tatu: Mama, watoto wote wanavaa hivi hivi siku hizi *(Ananung'unika).*
Mama: Hm. Haya sisi yetu macho tu. Maana husikizi tena. Umekuwa mkubwa, siwezi kukupiga.
Basi haya fanya utakavyo tu. *(Kimya).*
Tatu: Maa. *(Kwa hofu kidogo).*
Mama: Sema tu, nakusikia.
Tatu: (Ahema) Nataka ruhusa kwenda sinema.
Mama: Sinema gani?
Tatu: Empress.
Mama: Basi si bado? Leo ndio kwanza Ijumaa, "Lady Show" Jumapili.
Tatu: Nataka kwenda leo usiku.
Mama: Toka lini ukaenda sinema usiku? Siku zote unakwenda Jumapili mchana. Mchana sikukatazi, lakini usiku hapana, hapana, hata kidogo. Kwanza pesa za kukupa wewe kila Jumapili ziko wapi? Baba yako hali yake unaijua. Kila siku hapa analalamika kodi zimekuwa nyingi. Nawe unamsikia. Kodi ya kichwa, kodi ya miguu, kodi ya uzee, kodi ya mapato, kodi ya wafanyakazi, kodi, kodi, iiee! Nawe unataka sinema. Pesa zenyewe ziko wapi?

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Tatu: Mie sitaki pesa mama, nipe ruhusa tu. Swai atanichukua sinema. *(Ma Tatu ameshtuka.Anamtazama Tatu. Anarudia kusuka ukili wake).*
(kimya)
Tatu: Ma, atakuja sasa hivi. Jee nende? (kimya).
Mama:(Polepole) Na huyu Swai ndio nani?
Tatu: Mtoto mmoja Swai Hamisi. Najuana naye.
Mama: Mwanamume?
Tatu: (Anaitika kwa kichwa).
Mama: Nae anakuchukua sinema – Na kwa nini yeye akulipie sinema? Anakujuaje? Baba yako? Au nani? *(Anaacha kusuka)*
(Kimya).
Mama: *(kwa sauti ya juu)* Nijibu! Wewe unafikiri, anapata taabu hii yote ya kukuchukua sinema kwa nini, eh? Wewe mwana mzima sasa huwezi kufikiria?
Tatu: Mama ingekuwa kuna jambo lolote baya tusingetaka ruhusa. Swai ni rafiki tu.
Mama: Hakuna urafiki baina ya mtoto wa kiume na mwanamwali hata kidogo. Uwongo. Usitudanganye.
Hivi unaniona mjinga sana, eh?
Tatu: Mama *(kwa sauti ya kubembeleza)* siku hizi watoto wote wanakwenda na marafiki wa kiume
kutembea, si kitu geni.
Mama: Sio uzungu! Ndio kuiga uzungu tena. Basi sisi si wazungu. Mzungu na Mwafrika mbalimbali. Mila zetu mbalimbali. Wao hawana haya, anaweza kwenda na mume huyu na mume yule
isiwe kitu.
(Ebrahim Hussein, Michezo ya Kuigiza, Nbi: EAPH, 1980)

MASWALI

1. Pendekeza kichwa mwafaka kwa kifungu hiki. **(alm1)**
2. Taja wahusika **wawili** wa kiume waliorejelewa katika kifungu hiki. **(alm2)**
3. Taja sababu **nn**e zilizomfanya Mama amzuie Tatu kwenda sinema. **(alm4)**
4. Eleza tofauti kati ya mila za Wazungu na za Waafrika asilia kulingana na kifungu hiki. **(alm3)**
5. Huku ukitolea mifano kutoka kwenye kifungu, onyesha tabia **tatu** za Tatu. **(alm3)**
6. Ina maana gani kusema "Haya sisi yetu macho tu"? **(alm2)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 15)

1. Toa mfano mmoja mmoja kwa kila aina ya konsonanti uliyopewa. **(alm2)**

(i) Kipasuo:

(ii) Kitambaza:

2.(a) Taja vipashio vya lugha. **(alm2)**

(b) Rekebisha sentensi hii: Mwalimu ambaye aliyenifunza amekuja. **(alm2)**

3. Bainisha viambishi awali, mzizi na viambishi tamati katika maneno yafuatao: **(alm3)**

	Viambishi awali	Mzizi	Viambishi tamati
Atakutengenezea			
Wasaidieni			

4 Andika sentensi zifuatazo katika ukubwa.

(i) Wanawake hao waliuza mbuzi wao wote. **(alm1)**

(ii) Kigari chake kiliharibikia katika kibonde chenye kijito. **(alm2)**

5 Tunga sentensi kuonyesha tofauti ya <u>ki maana</u> kati ya maneno haya. **(alm2)**

(a) Vua: **(b)** Fua:

6 Utatafuta maneno gani kwenye kamusi, ukitaka kujua maana za maneno yafuatayo. **(alm1)**

(a) Kucheza:

(b) Usinipige:

SEHEMU C: USHAIRI (ALAMA 10)

Wapenda mtu kwa kitu

Shairi nakuleteya, tafadhali mwana twaa
Hikwita hunikimbiya, na kunitiya tama
Kumbe mebadili niya, hata washenzi watwaa
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Nilidhani u libasi, njema ya mtu kuvaa
Hawa sina wasiwasi, popote ninapokaa
Kumbe u mtu rakhisi, atakaye hukutwaa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.

Usinionye mija, miuja haitafaa
Kwamba huna nami haja, ukinambia si baa
Mtu hupenda kimoja, sende nami kwa hadaa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

Umejifunza wekevu, kutaka kunihadaa
Na huno wako uovu, ni bure hautafaa
Mimi ni wana mtuvu, sitendwi hataataa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.

Kunena mangi nataka, lakini wasaa
Na hapa tulipofika, ni kheri hakuambaa
Maana u mtu nyoka, huna ahadi u baa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.

Tamati sineni sana, muhibu toa tamaa
Ulotenda nishaona, wala hutanihadaa
Sasa kheri kuatana, kulla mtu akaa
Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu.
(Kutoka, Malenga wa Mvita, uk. 163)

Maswali

1. Shairi la mishororo minne katika kila ubeti huitwa? **(alm1)**
2. Tambua vina katika ubeti wa pili. **(alm2)**
3. Eleza maana ya 'Una mahaba tama, wapenda mtu kwa kitu,' **(alm2)**
4. Taja mambo **matatu** ambayo msemaji analalamikia katika shairi? **(alm3)**
5. Maneno yafuatayo yameendelezwa kishairi. Yaandike kwa njia sanifu: **(alm2)**
(a) hikwita:
(b) kuatana:

SEHEMU D: ISIMUJAMII (al.4)

(a) Isimu jamii ni nini? **(alm2)**
(b) Eleza mambo **mawili** anayozingatia mzungumzaji yeyote ili kutumia lugha inavyofaa. **(alm2)**

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 6)

(i) Kuna tofauti gani kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. **(alm 2)**
(ii) Eleza tofauti **mbili** kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. **(alm 2)**
(iii) Eleza tofauti kati ya: **(alm2)**
(a) Hekaya:
(b) Hurafa

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

FORM ONE HOLIDAYS SMART PASS
KISWAHILI KARATASI NAMBARI: 10

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Changamoto kubwa inayowakabili watu wengi katika mataifa yanayoendelea ni suala la chakula. Suala hili linaweza kuangaliwa katika sawia mbili tofauti. Kuna tatizo linalofungamana na uhaba wa chakula chenyewe. Uhaba huu unaweza kutokana na utegemezi mkubwa kwa zaraa kama nyenzo kuu ya uzalishaji wa chakula.

Zaraa katika mataifa mengi hususan yanayoendelea, hutegemea mvua. Kupatikana kwa mvua huathiriwa na mabadiliko ya tabianchi ulimwnguni. Matendo na amali za watu kama ukataji wa miti na uchafuzi wa mazingira huwa na athari hasi kwenye tabianchi hiyo. Mabadiliko ya tabianchi huweza kuvyaza ukama kutokana na **ngambi ya mvua**.

Kibinimethali kutokea wakati mafuriko yanapotokea na labda kuyasomba mazao mashambani na kusababisha baa la njaa. Hali hizi mbili husababisha matatizo makubwa ya chakula na kuathiri pakubwa suala zima la usalama wa chakula. Ili kuzuia uwezokano wa kuwepo kwa shida hii, pana haja ya kuwepo kwa mikakati na sera za kuhakikisha kuna usalama wa chakula. Kwa mfano, pana haja ya kukuza kilimo cha umwagiliaji ili kuepuka **adha** inayosababishwa na ukosefu wa mvua. Kwa upande mwingine, sharti zichukuliwe hatua mufidi za kuzuia na kupambana na athari za gharika.

Changamoto nyingine inahusiana na usalama wa chakula chenyewe. Chakula kilichosibikwa na vijasumu au kwa njia nyingine ile huweza kumdhuru anayehusika. Msibiko wa chakula unatokana na vyanzo tofauti. Mathalan uandalizi wa chakula kilichochafuliwa na choo, kutozingatia mbeko za usafi, uandaaji wa chakula na kukiweka katika hali ya uvuguvugu kabla ya kukipakua – hali inayochochea ukuaji wa viini na ulaji wa chakula kisichoandaliwa vyema. Ili kuepuka uwezekano wa kuathirika, pana haja ya kuzingatia usafi wa chakula na uandalizi unaofaa. Fauka ya hayo, vyombo cya uandalizi view safi, kanuni za usafi zifuatwe, upikaji na uandaaji uwe kamilifu. Hali hii isipozingatiwa, siha za raia wenyewe zitaathirika pakubwa.

Maswali.

1. Taja aina mbili za kuangalia suala la chakula katika mataifa yanayoendelea. **(alm2)**

2. Taja hatua mbili zinazoweza kuchukuliwa kupambana na tatizo la chakula. **(alm2)**

3. Eleza jinsi nne tofauti namna chakula kinavyoweza kuwa si salama? **(alm4)**

4. Kwa nini ni rahisi kukipakua chakula baada ya kukiandaa tu? **(alm1)**

5. Ni mapendekezo gani anayoyatoa mwandishi kuhakikisha kuwa chakula kinafaa? **(alm4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

MATUMIZI YA LUGHA

1. Kwa kutoa mifano eleza tofauti kati ya**:** **(alm 2)**

i. Silabi funge **ii.** Silabi wazi

2. Onyesha sauti zenye sifa zifuatazo**:** **(alm2)**

i. Kipasuo cha ufizi **ii.** Kikwamizo cha kaakaa laini

3. Tambua aina ya nomino katika sentensi zifuatazo**.** **(alm2)**

i. Mchanga hufanya miti kumea.

4. Bainisha mofimu katika kitenzi**.** **(alm2)**

Kilipikika

5. Tambua vivumishi katika sentensi ifuatayo na ueleze ni vya aina gani**.** **(alm2)**

i. Mtoto wake ameng'oka jino. **ii.** Msemo wenye tafsida hupendwa.

6. Andika kinyume cha: **(alm1)**

Tulinunua nguo aliizozianika jana.

7. Nomino 'uki' iko kwenye ngeli gani. **(alm1)**

8. Ainisha vitenzi kwenye fungo zifuatazo: **(alm3)**

i. Yatakuwa yangali yanakoma.

ii. Maria na Atieno ni wanafunzi watiifu.

9. Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo. **(alm2)**

i. Rais ametutembelea mara sita mwaka huu.

ii. Nendeni haraka shuleni.

10. Eleza maana inayojitokeza kwenye sentensi ifuatayo. **(alm1)**

i. Waiteni watu wale.

11. Tumia kiwakilishi kisisitizi kutungia sentensi ya wingi wakati uliopita. **(alm2)**

ISIMU JAMII

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Haya ng'ara … Ng'ara leo! Nguo motomoto. Ng'ara leo kwa bei rahisi. Hamsini hamsini shati. Kuona ni bure. Bure kwa bure. Shika mwenyewe ujionee. Bei nafuu. Bei ya starehe. Haya, haya. Usikose mwanangu! Hamsa! Hamsa! Fifty!Hamsa! Fifty! Hamsa na nyingine.

Maswali.

a. Bainisha sajili ya mazungumzo haya. **(alm 1)**

b. Eleza sifa nane za sajili hii kwa kurejelea kifungu hiki. **(alm 4)**

FASIHI SIMULIZI.

a. Fafanua maigizo. **(alm2)**

b. Ainisha kipera cha maigizo. **(alm4)**

c. Eleza sifa za maigizo. **(alm4)**

Prefer Calling Amobi Group of Examiners @ 0743 333 000 or 0706 851 439 for Marking Schemes

CALL AMOBI GROUP OF EXAMINERS @ 0743 333 000 OR 0706 851 439 TO ACQUIRE :











